

# MAREJEO YA 2016

ATD
FOURTH WORLD

**ATD Fourth World**
Usajili nº 003447 under NGO Act, 2002
S.L.P 61786, Dar es Salaam – Tanzania
Offisi number: 0222761717
atd.tanzania@gmail.com
https://www.facebook.com/ATDTanzania/
Kiingereza website: **http://www.atd-fourthworld.org/where-we-are/africa/tanzania/**
Kiswahili website: **http://www.atd-fourthworld.org/where-we-are/africa/tanzania/tanzania/**

# UTAMBULISHO

Tunayo furaha kuwaletea taarifa ya matukio muhimu, masimulizi na shughuri zilizotuhamasisha sote katika mwaka 2016.

Kupitia kwa wanachama, ATD Dunia ya Nne ilijikita kwa moyo, nguvu na juhudi katika kusaidia jamii kukabiliana na hali ya umaskini uliokithiri. Mwaka 2016 uliruhusu uhamasishaji wa nguvu wa wanachama wa ATD katika masuala mbalimbali ya elimu katika maeneo mbalimbali katika ukamilifu wake. Katika adhimisho la Siku ya Kutokomeza Umaskini Duniani, zaidi ya watu mia mbili walikusanyika ikiwa fursa kwa marafiki, familia na wanaharakati (watu wanaoishi katika umaskini uliokithiri, wakichukua majukumu katika harakati za shirika) wafanyakazi wa kujitolea wa kudumu wakiwakilisha na kutoa taarifa kuhusu harakati za kidunia.

Marejeo haya ya mwaka yana lengo moja: kushirikishana nawe mtazamo wa kidunia wa watu husika na kukuonesha mitazamo mbalimbali ya mapambano dhidi ya umaskini uliokithiri yanayoongozwa na Shirika kupitia wanachama wake.

Mwaka 2017 tutaadhimisha pamoja miaka mia moja ya kuzaliwa Joseph Wresinski, miaka 30 ya maadhimisho ya Siku ya Kutokomeza Umaskini Duniani na miaka 60 ya kuanzishwa ATD Dunia ya Nne.

Tuzidi kuwa pamoja.




CHAMPION

# ATD Dunia ya Nne...

## ... katika maneno machache

"Wote kwa Pamoja" inamaanisha umoja wa Harakati, vile vile umuhimu wa kuunganisha juhudi ya kila mtu kufikia malengo husika.

"Utu" unawakilisha msingi wa harakati za ATD. Wanachama wa ATD wanaoishi katika Umaskini uliokithiri  na marafiki wanaeleza kwamba Utu unahusu thamani ya kila binadamu, pamoja na heshima ambayo kila mtu anastahili. Utu unawakilisha kiini cha ubinadamu; kila mtu ana utu. Hata hivyo, katika kesi nyingi, binadamu hawaheshimiwi kama vile invyostahili.

ATD Dunia ya Nne ni harakati za kimataifa zilizoanzishwa nchini Ufaransa mwaka 1957. Sasa ipo katika nchi zaidi ya 30 duniani kote. ATD Dunia ya Nne imekuwapo Tanzania tangu mwaka 1999 jijini Dar es Salaam: Tandale, Tegeta (Kunduchi, Boko), Chasimba na Soko la Samaki Magogoni.

Watu wanaoishi katika umaskini uliokithiri ni lengo kuu la Harakati zetu, kushiriki kikamilifu katika ufumbuzi wa kuondokana na umaskini uliokithiri, pamoja tunasimamia haki za wote, kujenga uelewa kwa umma na ushawishi katika sera za umma.



# ATD Dunia ya Nne mwaka 2016

## Nini utakacho kiona katika mrejeo huu?

Tafadhali gundua mambo mbalimbali ya shughuri zinazoratibiwa na ATD Dunia ya Nne na wanachama wake kwa mwaka 2016. Mwaka huu llicha ya uwanda mkubwa wa shughuri nyingi, matukio na mafanikio yaliyofikiwa 2016, unakaribishwa kugundua watu na wanachama walioifanya ATD leo ionekane kuwa ni nini katika Tanzania.

Utaona maelezo kuhusu huduma maalumu za taswira za mwaka uliopita. Karibu sana.


**Kupata Haki /** Elimu kwa Wote ....................................................9

**Kupata Haki**_/ Vyeti vya Kuzaliwa ................................................ 11

**Kupata Haki**_/ Elimu Ya Watu Wazima ......................................... 11

**Kimataifa** / Mkutano wa Bangui .................................................... 13

**Watoto** / Maktaba ya Mtaani ..........................................................13

**Mabadiliko katika ofisi** / Kwa hatua mpya .....................................15

**Familia** / Uwepo na kusaidiana ..................................................... 15

**Vijana** / Kikundi cha Vijana Marafiki ............................................... 17

**Matukio** / Siku ya Kutokomeza Umaskini Duniani ............................ 19

**Vijana** / Semina ya Kanda ya Vijana ............................................... 21

**Utafiti wa Vipimo vya Umaskini** / Kuzinduliwa ................................23

**Muhtasari wa matukio** / Kumbukumbu katika picha ....................... 24

**Mwito wa Kuchukua Hatua** / Kampeni ya 2017 ...............................33

**Tutakuwa wapi kesho** / Malengo yetu ya pamoja ........................... 34



# UPATIKANAJI WA HAKI ZA

## Elimu kwa wote

**Upatikanaj wa elimu kwa watoto wanaoishi katika umaskini uliokithiri.**
*“Elimu hunisaidia kufikia malengo yangu. Elimu ni ukombozi kwa maisha yangu, familia yangu na jamii yangu”.”Elimu ya msingi ni haki ya kila mtoto bila ya kuangalia hali au tamaduni ya jamii fulani”.* Ukosefu wa haki hii ya kupata elimu kwa watoto wanaoishi katika umaskini uliokithiri huzifanya familia nyingi kuwa katika hali ya unyonge.


Mwaka 2016 mwezi wa tatu ATD ilikamilisha mradai wa utafiti. Kundi la utafiti wa Elimu kwa Wote ilikamilisha kipindi cha kufanya utafiti ambao ulifanyika kwa muda wa kipindi cha mwa mmoja na nusu. Utafiti uliambatana na mada sita tofauti kufuatana na maisha ya watu: Binafsi, Afya, Makazi na Jamii, Fedha, Shule na familia na marafiki. Taarifa zilikusanywa na kutolewa kwa pamoja na kuchambuliwa kutokana na kila mada kisha kukapatikana matokeo ya utafiti. Matokeo ya utafiti yaliweza kuleta Mapendekezo kumi na tano yaliotokana na mchango wa watu wote waliohojiwa.

**Semina:** Mwaka 2016 mwezi wa sita kundi la utafi lilifanya mkutano mkubwa wa uwakilishaji wa taarifa ya utafiti na kuwakilisha matokeo ya utafiti. Walishiriki watu kutoka katika matabaka tofauti, walimu wakuu wa shule za msingi, wazazi, viongozi, maafisa elimu na wadau wengine mbali mbali wa elimu. Mwishoni mwa mwaka 2016 tulijadili mipango na mikakati ya kuelekea mwaka 2017 ikiwemo kusambaza matokeo ya utafiti na kuwaleta wadau mbali mbali wa elimu kwa pamoja na kujadili haki ya upatikanaji wa elimu ya msingi kwa watoto wanaoishi katika umaskini uliokithiri. Katika utekelezaji wa hili kutakuwa na mikutano itakayowaleta pamoja wazazi, walimu na viongozi wa serikali za mitaa, mikutano ya shule na kujadili haki za msingi katika elimu ya shule ya msingi. Mchakto huu utaendeshwa na timu ya elimu kwa wote inayoundwa na walimu, watu wanaoishikatika umaskini na wanaharakati wa kujitolea wa ATD Dunia ya Nne.




Ice Cold
Coca-Cola





## Vyeti vya Kuzaliwa

For the last year the ambition was to continue supporting families living in extreme poverty to get birth certificates for their children in specific areas of Dar es Salaam: Boko, Kunduchi and Tandale. We were looking for a new way in order to support them and as well other families in their community. Last year 64 children were registered and succeeded to get birth certificates.

People living in poverty at Kundunchi, Chasimba, Boko are supporting families: giving information, helping to fill the forms and be the contact with ATD Fourth World. The success of the project depends as well from the support of RITA's staff after many years of contact. As with any action aimed at accessing rights for the most excluded, everything is possible when citizens and institutions work together.

When families get the birth certificate they feel proud and hope for the future of their children. A birth certificate is a basic right and a key to fight exclusion from the society. ATD Fourth World will follow the project in 2017.

Kupata Haki

## Elimu Ya Watu Wazima

From July to November 2016 nearly twenty people attended a class regularly to learn how to read and write Swahili in the heart of the Fish Market, in the meeting room of the board of administration. Thanks to their support, three afternoons a week, two teachers from Ilala Education District facilitated the class. The learners experienced a new method called "Ndiyo Ninaweza" (Yes I Can), based on the experience for teaching adults. The group was composed of adults and young people having in common no chance as a child to follow primary school education. They left behind the shame that one could feel and showed strength and courage.

The class, implemented close to their place of living and working showed that with good conditions to learn, people can succeed, whatever the conditions of life.

The learners really lived a common story where they got to know each other. One of the youngest learners said: *"We feel as a family, really. We meet together, we exchange, we support our neighbour. If someone misses one day we try to show him. We try to progress together".*









## Mkutano wa Bangui

Katikati ya mwezi Julai mwaka 2016, Rehema Jakson Mapunda, Mbaraka Ramadhani Kilima na Salehe Musa Seif waliiwakilisha ATD Dunia ya Nne Tanzania wakiwa miongoni mwa wanachama 40 wa ATD walioungana kutoka nchi saba barani Afrika, na wajumbe wa kanda ya Afrika, walikutana Bangui Jamuhuri ya Afrika ya Kati kwa ajili ya mkutano mkuu wa kikanda. Mada mbili zilijadiliwa, nazo ni: "dhamira ya kujitolea kwa moyo wote kutomuacha mtu yeyote nyuma " pamoja na majukumu muhimu "kutekeleza majukumu ya shirika kwa pamoja". "Ni muhimu kwa marafiki, watumishi wa kujitolea na wafadhiri wa ATD Dunia ya Nne kujuana na kusaidiana kufanya harakati zisonge mbele ambapo hakuna atakae achwa nyuma. Kuungana kwetu pamoja kunatoa fursa ya kusaidiana kwenye udhaifu na uimara wetu ili kupata nguvu itakayotuwezesha kuwafikia watu wengi waliotengwa.

Sisi kama wanaharakati wa kimataifa na wote tunatoka katika tamaduni mbalimbali, tukutanapo hujifunza kuaminiana na kutegemeana kikamilifu licha ya tofauti zetu kubwa tulizonazo.



## Maktaba

Katika Maktaba ya Mtaa ya Tandale, Kila Jumatano alasiri, watu wanaojitolea na marafiki wa ATD huwezesha shughuli mbalimbali wakiwa pamoja na watoto. Katika maeneo hayo na jirani zaidi ya watoto sitini walio na umri kati ya mwaka 1 hadi 14 hushiriki katika Maktaba ya Mtaa kila wiki. Sisi hukaribisha marafiki watatu wapya kwa uhuishaji: Pelagie, Margret na Rajab.

Maktaba ya mtaa ni mahali kwa ajili ya watoto kushirikiana ili kujenga urafiki na wale wasio na marafiki na kucheza na kujifunza kwa wakati mmoja. Ni mahali pa kuwandaa wale ambao bado hawajajiunga na shule, wakati wa watoto waliotoka katika mazingira tofauti kuwa pamoja, kucheza pamoja, kushirikiana vifaa mbalimbali na watoto wengine. Wakiwa pamoja hufurahia mambo mengi kama vile vitabu na hadithi tofauti. Maktaba ya Mtaa ni wazi na huru, katka kuhakikisha mtu yeyote anaweza kushiriki. Pia Maktaba ya mtaa ni nafasi kwa ajili ya wazazi na watoto ambapo wanaweza kuja na kushiriki kile wanachokijua na kufurahia pamoja.








# *Mabadiliko katika ofisi*

## Kwa hatua mpya

Tangu Novemba mwishoni, timu yetu imeendelea kukua. Tumeendelea kuwakaribisha wanachama wapya ambao ni maalum watakaojihusisha katika utafiti wa kubaini vipimo vya umaskini na jinsi ya kuvipima. Mikutano ya mara kwa mara huandaliwa ikiwa ni sehemu ya utafiti. Pia imekuwa ni muhimu kupanua ofisi ili kuwa na nafasi ya kuweza kufanya kazi kuendana na mabadiliko mapya.

Chumba kipya kilijengwa, na ilitupa nafasi ya kufanya baadhi ya kazi zinazohusiana na ofisi . Tulibadilisha paa, na vyumba viwili vya ofisi viliwekwa marumaru. Upakaji wa rangi ulifanywa pia na wanachama wa timu. Pia tuna nambali mpya za mawasiliano, ambazo ni:
**022 276 1717**.

Tumeridhishwa na mabadiliko haya ambayo yameifanya ofisi ya ATD kupendeza na kuvutia zaidi.. Kazi bado haijakamilika na tumepanga kuandaa siku ya kazi ya jumuiya ambapo kila mwanachama wa harakati ataweza kushiriki.

# *Familia*

## Uwepo na kusaidiana

Kitu muhimu zaidi katika njia ya utendaji wa ATD ni kuwa karibu sana na familia zinazoishi katika umaskini uliokithiri. Wanachama wa ATD Dunia ya Nne waliitembelea famila moja ambayo ilisema: “Mnapo tutembelea, hujisikia kama watu wenye thamani ndani ya jamii., tunaosikilizwa na kutambuliwa katika juhudi zetu”

Kwa njia ya kutembelea na kuonekana Shirika linaweza kupata uelewa mzuri zaidi wa shida zinazowakabili watu kukabiliana na changamoto za kila siku. Familia inapowakaribisha wanachama wa ATD, uhusiano huongezeka na kuwa imara zaidi. Hali ya kuaminiana huimarishwa zaidi na pia kama marafiki tunaweza kutambua kwa pamoja nini cha kufanya kuunga mkono juhudi za kila mmoja.

Mara nyingi umaskini uliokithiri humaanisha maisha ambapo umeachwa nyuma. Kuwa karibu na watu katika maeneo yanayoishi ni njia ya kuvunja mduala wa kutengwa.




IYF

# Kikundi cha Vijana Marafiki

Kina nani marafiki vijana wa ATD…. kundi la vijana kuanzia miaka 18 hadi 25, baadhi wana ufahamu na uzoefu wa changamoto za umaskini kwa kila siku, wengine wanatoka katika familia zilizo na mazingira imara, lakini kila mmoja katika njia yake ya kipekee amejitoa kutafuta jinsi ya kubadilisha jamii yake kwa faida ya wote.

Nini maana ya kuwa Rafiki kijana wa ATD walituambia: *"...nikuona maoni ya watu na kumpatia nafasi kila mmoja kuongea; kujifunza kutokana na uzoefu wetu na kubadilika sisi wenyewe; kuheshimu, kuamini na kujenga urafiki na watu wengine na kuwambia wengine maana ya urafiki. Kuwa kijana wa ATD ni kuwa rafiki wa watu maskini sana kila mahali".*

Jinsi gani vijana wanahusisha wao wenyewe katika ATD…katika kila hatua za harakati Tanzania wanawakilisha, wanashiriki miradi mbali mbali ya utafiti na kusaidia. Kuendesha maktaba ya mtaa, huleta ubunifu, vichekesho na ngoma katika matukio ya kitaifa, hukuza hamu yao kwa kujifunza kwa kupitia, utamaduni: na wakisaidiana wao kwa wao na pale wanapopatwa na matatizo na katika vipindi vya furaha.

Nini mtazamo wa vijana marafiki katika kupambana na umaskini. Pazi kutoka kundi la vijana alisema, *"Mwanzo nilifikiri umaskini ni kutokua na pesa za kutosha kwa ajili ya chakula, nguo na malazi. Baadae nilienda mbali kiufahamu, nilijifunza kumbe ni kutengwa, na kunyimwa kushirikishwa katika jamii".*

Ushirikiano wao na kukataa kutengwa hujenga amani ndani ya jummiya zao na kuleta tumaini kwa kizazi kijacho.





# Matukio

## Siku ya Kutokomeza Umaskini Uliokithiri Duniani

Siku ya Kutokomeza Umaskini Ulkiokithiri Duniani kwa mwaka 2016 ilikusanya pamoja mamia ya watu jijini Dar es Salaam katika kijiji cha Makumbusho. Kauli mbiu ya mwaka huu ilikuwa *“Ushirikishwaji wa watu wote ili kutokomeza umaskini katika aina zake zote”* ili kuhakikisha kwamba watu wanaoishi katika umaskini uliokithiri wanakuwa washirika wa kwanza katika kila jambo katika maamuzi na miradi.

Mwaka huu kamati ya Oktoba 17 ilitaka kutoa taarifa kwa wajumbe wa ATD, familia na marafiki ambao mara nyingi walisema *“Kwa kweli hatujui hasa shirika linafanya nini katika kipindi cha mwaka mzima”.* Familia kutoka maeneo mbalimbli, marafiki, maafisa elimu, wanaharakati na wafanyakazi wa kudumu wa kujitolea, walitoa shuhuda, changamoto na mafanikio kwa yale yanayoendeshwa na shirika hapa Tanzania.

Kwa kila hatua shuhuda zililenga suala zima la ushirikishwaji kwa wale ambao walikuwa hawawezi kusikika na kuwawezesha kushiriki. Kwa mfano, familia zilizopata uzoefu wa kupata vyeti vya kuzaliwa zinaweza kushirikishana ujuzi wao na wengine pia kusaidiana. Wana – ATD wanaoishi katika umaskini uliokithiri, kuratibu kwa pamoja mradi wa Elimu kwa Wote na kuchangia ufahamu wao ili kuhakikisha hitimisho imara katika msingi wa ukweli na uhusishwaji wa wazazi na watoto katika upatikanaji wa elimu ya msingi.

Siku ya kutokomeza Umaskini Duniani inabaki kuwa siku ya kuadhimishwa pale mmoja anapojumuika kuionesha jamii kwamba zipo harakati za kizalendo zinakua ambazo zinakataa watu kuachwa nyuma. Mwaka 2017, kote duniani tutaadhimisha fursa ya kutoa mipaka mipya na kuitahadharisha jamii. Katika tukio hilo mwito kwa watu wote kuchukua hatua utazinduliwa mnamo 12 Februari, 2017. Angalia ukurasa 37.





# Semina ya Kanda ya Vijana

Tangu tarehe 20 hadi tarehe 25 Mwezi wa Tatu 2016, jumla ya vijana thelathini kutoka Kenya Tanzania, Ethiopia na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo walikutana jijini Dar-es-salaam Tanzania. Hii ilikuwa ni mara ya kwanza kwa tukio la aina hii kimataifa kwa ATD Tanzania tangu harakati zilipoanzishwa hapa nchini. Kila mkutano ni fursa ya kuimarisha dhamira ya kila mmoja wetu kwa ajili ya baadaye. Sehemu ya imani yetu, mashaka yetu na shauku zetu.

Wakati huu watendaji wakuu walikuwa vijana na moyo wa semina marafiki hakika ni mafanikio makubwa, na ni mafanikio yanayosaidia kujenga amani.

Kama alivyosema mmoja wao *“Mafanikio yoyote au maendeleo ya dunia yako mikononi mwetu kama vijana, dunia ambayo haitakuwa na ubaguzi, dunia bila umaskini. Lakini hilo litawezekana tu endap[o tutabaki tukiwa tumeungana. Endapo tungekuwa hatukuungana, huu mkutano hapa Dar es Salaam usingefanikiwa. Nilijifunza kujihusisha na matatizo ya wengine, hili ni tatizo langu na nina haki ya kuwasaidia wengine kufanikiwa. Ni kutokana na haya tunapokuwa marafiki wa wasio na marafiki”.*

Semina iliwathibitishia washiriki wote kwamba wanachokifanya ni thabiti nao walipata uhakika na fahari kwamba *“Vitu vidogo ambavyo kila mtu hufanya hatimaye huwa vikubwa”.* Kuwa rafiki wa asiyekuwa na rafiki, haya ni mafanikio ya kweli, na mafanikio haya husaidia kujenga amani.

Ulikuwa kuimarisha ahadi za vijana kuchukua hatua katika jamii zao na kuongeza shauku za vijana ambao pamoja nao hubeba msukumo wa kuleta mabadiliko.

Ally alisema, *“Pamoja na vijana kutoka mataifa mengine tumekuwa na ushirikiano mzuri, kama vijana, mnapokaa pamoja mnajenga upendo. Hii inatuwezesha sisi vijana kufanya makubwa zaidi ya nilivyotegemea”.*




Siku ya
kuutokomeza
umaskini
uliokithiri duniani
Kuungana pamoja ili kuhakikisha kwamba hizi haki
zinaheshimiwa ni jukumu letu sote.

# Utafiti wa Viashiria vya Umaskini

## Uzinduzi wa Mradi

**The Poverty Indicators study** is a research project to understand what poverty is, its dimensions and how to measure them. It is an opportunity to engage the intelligence of people trapped in poverty and to rethink with them what is poverty and how to measure it together with other participants like academics, policy makers or social workers. The Merging of Knowledge method will be employed in which people facing extreme poverty and social exclusion will be empowered to exchange ideas with other participants and be recognised as co-researchers, on an equal footing.

ATD Fourth World Tanzania is collaborating with the International Movement based in Mery-sur-Oise (France) and Oxford University (U.K) in this study. The study team is composed of ATD Tanzania members: people living extreme poverty who are active in the actions of the Movement, practitioners and academics engaged for the period of the project.

The research will follow the deep culture of the preoccupation for the respect of dignity and human rights, especially for people living extreme poverty starting from their experience, and the contributions of those who live daily exclusion.

The conclusions of the study will enable people and institutions involved in fighting against extreme poverty to understand what people really live in order to take good decisions.



# KUMBUKUMBU KATIKA PICHA








ASIYESIKIA LA MKUU
kijana Jabir ambaye alikosa usikivu kwa wazazi wake.
tabia zisizofaa za udokozi. Siku moja anakutana na tukio
hatimaye linabadilisha maisha yake kabisa. Ni tukio gani hilo?
MARIAM ABDI
Mkuki na Nyota Publishers Ltd









ATD
ATD
ATD





# The Call To Action Campaign

With events on three continents, the International Movement ATD Fourth World launched its global Stop Poverty campaign on the 12 February, 2017. It highlights people living in extreme poverty as full partners in the fight to end poverty.

*"Too often the suffering people living in poverty face is used to instil fear, to call for walls to be built, and to reject foreigners,"* Cassam Uteem, President of ATD Fourth World and former President of Mauritius said. *"In 2017, we want to tell the world about someone* (Joseph Wresinski) *who started a movement to unite people – those who live in poverty and those who do not – in order to eliminate obstacles that keep some people at the bottom".*

All year long we invite all of you to join the call to say Stop Poverty. You will be proposed to sign, give your voice, leave your testimony. Ask around to other ATD Fourth World members, share with your family, friends, neighbors to join the call. In 2017, we will celebrate as well the 100th birthday of Joseph Wresinski on the 12 February and the thirty years of the World Day for Overcoming Extreme Poverty.

If you have access to internet:
http://www.atd-fourthworld.org/stop-poverty/call-to-action/

ATD FOURTH WORLD

STOP POVERTY

ALL TOGETHER IN DIGNITY

## *Utangulizi “Nitakuwa wapi kesho”*

Kutokuwa na sehemu maalum ya kuishi, hofu kila siku nitakula nini. Kudharauliwa na mbaya zaidi kuonekana hawana thamani, elimu duni, watoto kutokwenda shule, kukumbwa na magonjwa mbali mbali, kufikiri kwamba kila wanachokifanya hakiwezekani. Haya ndio maisha ya watu maskini, hayana mwelekeo na huendelea kujiuliza licha ya juhudi zao zote, “*Nitakuwa wapi kesho?*”

*Japokuwa umaskini ni janga kubwa ni kama mtu aliefumbwa mdomo na kushindwa kuongea, Lakini ni watu ambao huweka juhudi zao katika kuijenga dunia yenye amani na kuweza kuishi katika hali ya usawa na kutambulika kwa watu wengine.*

## *Malengo*

**Thamani ya binaadamu wote ni sawa- kipaumbele kwa maskini**

Kipaumbele cha ATD Dunia ya Nne ni kwenda hatua kwa hatua, bega kwa bega, na watu maskini katika vitu vyote tunavyofanya. Ili kujenga uaminifu, ushirikiano mzuri na kuifungua mioyo, akili zetu na kujuana vizuri na kuendelea kuwatafuta watu wengine wasiokuwepo. Tunapaswa kuheshimu na kuzingatia vikwazo wanavyokutana navyo kila siku na kuitia moyo jamii kujua juhudi na namna ya kujenga jamii nzuri.

**Kujifunza katika maisha**

Ni ile shauku ya kujifunza kutoka kwa watu wanaoishi katika hali ya umaskini katika rika zote haiwezi kupungua. Ukiangalia maisha magumu wanayo kumbana nayo. Kiundani uelewa wetu ni juu ya sura nzima ya elimu na kujifunza maisha,huanzia nyumbani katikaka jamii, shuleni na kwa ujumla kwenye maeneo yanayotoa elimu. Kipaumbele  kitakua kutambua zile juhudi wanazozifanya watu wanaoishi katika umasikini na vikwazo wanavyo kumbana navyo katika kufanikisha suala la ujuzi. Lazima kuwasisitizia kujifunza kwa furaha na kuwatia moyo kwa kushiriki katika mafunzo yao na si kwa kufanya mashindano.

**Vijana – ndio taifa la kesho**

Katika kipindi cha ujana ni kipindi ambacho kila mmoja anataka kuonekana kuwa ni mtanashati na kujionyesha mbele za watu, lakini hukabiliwa na majukumu mazito ya kusaidia familia zao. Tutaendelea kuwatia moyo vijana kutoka matabaka tofauti kujitambua na kutimiza ndoto zao. Kuhakikisha kuwa juhudi zao zinatambulika katika jamii zao kama kujenga amani na kujenga taifa lao.

**Dunia ni ya wote**

Harakati zetu, mtazamo wetu, ni kwa dunia, kwa maskini na matajiri, kwa binaadamu wote kuishi kwa amani, umoja, utu na njia nzuri ya maisha. Tutawawezesha watu kufahamu na kuzifikia haki zao za msingi. Katika kueneza ujumbe tutashirikiana mitazamo, kwa kuanza na majirani, jamii yetu na walio mbali. Tutadumisha mshikamano na kuunda urafiki baina ya watu na makundi na kupeana ufahamu, mawazo na ujuzi tulionao kwa manufaa ya wote.



**ATD Fourth World**
Usajili nº 003447 under NGO Act, 2002
S.L.P 61786, Dar es Salaam – Tanzania
Namba ya Ofisi: 0222761717
atd.tanzania@gmail.com
English website : http://www.atd-fourthworld.org/where-we-are/africa/tanzania/
Kiswahili website : http://www.atd-fourthworld.org/where-we-are/africa/tanzania/tanzania/

https://www.facebook.com/ATDTanzania/

AGENCE FRANÇAISE DE DÉVELOPPEMENT